Jarida La Februari
REVIVAL NEWS
From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

FEBRUARI 2021 ** FEBRUARI 2021 **** FEBRUARI 2021 ****

BETHLEHEMU
NYUMBA YA MKATE

Nicholas Jackson

Kuna hazina nyingi katika neno la Mungu. "Ni utukufu wa Mungu kuficha jambo; bali ni utukufu wa mfalme kuchunguza jambo!" Mithali 25:2. Katika kipindi cha juzi cha kufundisha cha Januari, tuliamua kwa mara ya kwanza kufanya uchunguzi wa mahali "Bethlehemu" katika Bibilia yote. Kwa kufanya huu uchunguzi kutumia Strong's Concordance tumetajirishwa na hazina za ajabu ambazo zimegunduliwa! Ndiyo hii sehemu ya ujumbe ambao Mungu anao kwetu kuhusu "Bethlehemu".

Maana ya "Bethlehemu"

Neno Bethlehemu ni neno ambalo limeundwa kwa sehemu mbili: Beth na Lehemu. Neno Beth linamaanisha nyumba na linaweza kumaanisha nyumba kwa njia ya jengo au familia. Lehemu linamaanisha chakula, hasa nafaka au mkate. Pamoja Bethlehemu linamaanisha Nyumba ya mkate au Nyumba ya Chakula. Tunajifunza juu ya nyumba ya chakula! Ni mahali pa utoaji; mahali pa chakula; mahali ambapo unaweza kupata mkate!

Yesu, Mkate wa uzima, alizaliwa Bethlehemu

Kitu ambacho kinafahamika sana kuhusu Bethlehemu ni kwamba huko ndiko Yesu aliye Masiha alikozaliwa. Katika Yohana 6:35 &48, Yesu alitoa tangazo la ajabu, "MIMI Ndimi Mkate wa Uzima!" Mkate wa Uzima ulizaliwa katika hii dunia kwenye Nyumba ya Mkate! Kuna chakula, utoaji na mkate katika Nyumba ya Mkate! Tukiula huu Mkate, "tutaishi milele" Yohana 6:51. Watu leo wanaweza kupata Mkate wa Uzima, ndani yetu, watu wake. Kanisa linafaa kuwa Nyumba ya Mkate ambapo dunia inaweza kupata Mkate wa Uzima na kuishi milele! Dunia bado inaweza kumpata Yesu katika Nyumba ya Mkate, Bethlehemu, "nyumba ya kweli" ya Mungu, ambayo ni kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli" 1 Timotheo 3:15. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kulipokuwa na umati wa watu walo na njaa, "wapeni ninyi vyakula!" Mathayo 14:16. Wanafunzi wanafaa kusambaza mkate ili wote waweze kula na kushiba!

KUTAJWA KWA BETHLEHEMU KWA MARA YA KWANZA

Neno Bethlehemu linajitokeza mara ya kwanza katika Mwanzo. Kitabu cha Mwanzo ni kitabu cha mianzo na kweli nyingi za milele za Mungu zinapatikana kwa hali ya mbegu katika kitabu hiki, kufunua kusudi la Mungu la milele. Bethlehemu sio tofauti! Kutajwa kwanza ni katika Mwanzo 35:19 "Akafa Raheli, akazikwa katika njia ya Efrathi, ndio Bethlehemu"

Mahali pa kuzaa matunda

Muktadha wa huku kutajwa mara ya kwanza ni wa ajabu. Katika Mwanzo 35:16 inasema kwamba Yakobo na familia yake walikuwa wakisafiri kutoka Betheli kwenda Efrathi na kwamba "Raheli akashikwa na utungu wa kuzaa, na utungu wake ulikuwa mzito". Neno hili Efrathi hujitokeza mara nyingi na Bethlehemu na humaanisha: kuzaa matunda, jina jingine la Bethlehemu (maana kutoka kwa Strong's Concordance). Maelezo mengine ni fungu la majivu: mahali pa kuzaa matunda (maelezo ya BDB). Bethlehemu pia linajulikana kama Efrathi au Efrati na ni mahali pa kuzaa matunda; kuzaa matunda ambao unatokana na fungu la majivu! Kwa maneno mengine, ni kuzaa matunda ambao unatokana na shida, hali ngumu, maangamizi na tanzia. Kulikuwa na utungu mzito wa kuzaa kwa Raheli kuleta tunda la mwana.

Kifo cha Raheli

Katika Mwanzo 35:17-18 Raheli alikuwa kwa utungu mzito kuleta mwana, "Ikawa hapo katika kutoa roho yake (maana alikufa)". Raheli alikuwa nani? Raheli alikuwa mke mpendwa wa Yakobo. Alikuwa mke ambaye Yakobo alifanya kazi ili apewe. Alikuwa mke wa upendo wake. Lakini ili kuona huyu mwana amezaliwa, mke wa upendo wake alikufa. Kuna picha la kinabii hapa: kutoka kwa majivu ya kifo cha Raheli kulitokea mwana! Yesu alilia juu ya Yerusalemu, mke mpendwa wa Yahweh (Ezekieli 16:1-14), "Angalieni, mmeachiwa nyumba yenu!" Luka 13:35. Yesu alinena kuhusu hukumu ya na taifa la Israeli iliyokaribia, lakini kutoka kwa uharibifu na majivu yake kungetokea Mwana!

Mwana wa huzuni yangu, Mwana wa Mkono wa Kuume

Roho wa Raheli ilipokuwa ikitoka aliambiwa namkunga, "Usiogope, maana sasa utamzaa mwanamume mwingine" Mwanzo 35:17. Kisha alipokuwa akifa "akamwita jina lake Benoni; lakini babaye alimwita Benyamini" Mwanzo 35:18. Benoni linatafsiriwa kutoka kwa Kihibrania kama Mwana wa huzuni yangu. Jina Benyamini linatafsiriwa kama Mwana wa mkono wa kuume! Mwana ambaye alitokana na kifo cha Raheli ni mwana wa huzuni yangu na pia ni mwana wa mkono wa kuume! Hii ilifanyika "Efrathi (yaani Bethlehemu)"19.

Mwana wa huzuni

Wakati Israeli kuhangaika kama taifa, Mwana alizaliwa! Alizaliwa Bethlehemu, nyumba ya mkate. Angekuwa Mwana wa huzuni yangu na pia Mwana wa mkono wa kuume! Neno huzuni ni neno la Kihibrania aven linalomaanisha: shida, uovu, dhambi. Yesu Masiha angekuwa Mwana ambaye angebeba uovu wetu wote, shida na dhambi! Alitabiriwa katika Isaya 53:3 kama "Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko"! Yesu ndiye Mwana aliyebeba huzuni yetu! Huyu mtu alikuwa kama "mche mwororo, kama mzizi katika nchi kavu" Isaya 53:2. Alitokea kwa kitu kilichokufa. Alitokea kwa majivu! Alizaliwa kutoka kwa taiafa lililokauka, lenye ukiwa na lililokufa kwa Mungu!

Mwana wa Mkono wa Kuume

Yule mmoja aliyekuwa Mwana wa huzuni pia ni Mwana wa Mkono wa Kuume! Yule aliyechukua huzuni yetu na uovu katika msalaba ndiye yule pia ambaye "alifufuliwa katika wafu akawekwa kwa mkono wa kuume katika ulimwengu wa roho, juu kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani…" Waefeso 1:20-21. Raheli alipomwona mwana alisema, Mwana wa huzuni yangu. Lakini baba yake, Yakobo, akaingilia kati na kusema, Mwana wa mkono wa kuume. Yesu alijinyenyekeza kuwa Mwana wa huzuni na kwa hivyo Mungu

“alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina” Wafilipi 2:9. “Yahweh alimwambia Bwana wangu, ‘Uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako” Zaburi 110:1.

Yule aliyezaliwa Bethlehemu, Nyumba ya Mkate, ndiye Mwana wa huzuni ambaye alikuwa Mwana wa Mkono wa Kuume!

RUTHU-nja katika nchi

Katika nyakati za waamuzi, “kulikuwa na njaa katika nchi” na familia moja ya “Waefrathi wa Bethlehemu, Yuda” walitoka Bethlehemu “akaenda kukaa katika nchi ya Moabu” (Ruthu 1:1-3). Waliacha Nyumba ya Mkate, Bethlehemu, kwa ajili ya njaa. Kulikuwa na njaa katika nyumba ya Mkate! Katika ulimwengu wa kanisa la leo, hivi ndivyo hali imekuwa. Watu wameacha kile kinachoitwa “kanisa” kutafuta mkate kwa sababu hakuna cha kula; hakuna neno la kulisha na kutia nguvu. “Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu” Mathayo 4:4. Mkate ni Neno. Kunafaa kuwa na mkate katika kanisa. Wengi wameenda nje kutafuta mkate katika nchi ya ugeni kwa sababu haukupatikana katika mahali ambapo panaitwa “kanisa”.

Yahweh akatembelea kwa kuleta mkate

Baada ya uharibifu wa kupoteza mume wake na wana wawili, Naomi “alisikia ya kwamba Yahweh amewajilia [hasa amewashughulikia] watu wake na kuwapa chakula” Ruthu 1:6. Mkate umerudi katika Nyumba ya Mkate! Watu wakisikia kwamba, kuna chakula katika nyumba ya Mungu tena, tutaona wengi wakimrudia Yesu nyakati hizi, wakiwa wamekonda na wana njaa, wakitafuta mkate wa kweli unaotosheleza! Kuna ufufio wa Neno. Yahweh huwatembelea na kutushugulikia kwa kutupa mkate wa Neno lake!

Mataifa kurudi

Naomi alipoamua kurudi, mkaza mwana wake, Ruthu, Mmoabi, alishikamana na Naomi kwa kiapo cha agano, “watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu” Ruthu 1:16. Kwa hivyo kuna Myahudi, Naomi, na Myunani, Ruthu, wakirudi Bethlehemu! “Basi Naomi akarudi; pamoja na Ruthu, Mmoabi…wakafika Bethlehemu” Ruthu 1:22. Myahudi na Myunani kuja kula pamoja katika Nyumba ya Mkate. Kukiwa na mkate wa kweli katika nyumba, hatubaki tumegawanyika tena, kwa maana, “sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sote twapokea sehemu ule mkate mmoja”1Kor.10:17.Myahudi na Myunani kuja pamoja Bethlehemu kushiriki Mkate mmoja, Yesu aliye Masiha, Neno lililofanywa mwili!

Kuna mavuno Bethlehemu

Naomi na Ruthu walirudi Bethlehemu “mwanzo wa mavuno ya shayiri” Ruthu 1:22. Mwanzo wa mavuno ya shayiri ulikuwa kipindi baada tu ya malimbuko na ulikuwa kipindi cha wiki saba katikati ya pasaka na pendekote. Huu ndio wakati wa kinabii wa mavuno ya mioyo kuja katika ufalme, kuamini Yesu kama mwanakondoo wa Pasaka, kuamini ufufuo wake kama malimbuko (1Kor.15:20) na kisha kuingia mapito ya Pendekote, kujazwa na Roho Mtakatifu. Naomi na Ruthu walikuja Bethlehemu katika mwanzo wa mavuno! Kama mtoto mchanga, Ruthu anaenda nje “akaokota masazo nyuma ya wavunaji” Ruthu 2:3. Ruthu alikuja Bethlehemu na kuingia moja kwa moja katika kazi ya mavuno, kuona wavunaji na kuokota masazo. Alikuja kwenye

picha ya kanisa linalotenda na kufanya kazi wakati wa mavuno na alikuwa anaokota nafaka na kulisha mama mkwe wake!

Boazi-Bwana wa mavuno

"Na tazama, Boazi akaja kutoka Bethlehemu kawaamkia wavunaji, akasema, Bwana akae nanyi. Nao wakamwitikia, Bwana na akubariki!" Ruthu 2:4. Boazi alikuwa Bwana wa shamba hili na juu ya wavunaji. Yesu alituambia "Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake" Mathayo 9:37-38. Yesu huwatuma watenda kazi na wavunaji katika mavuno yake. Yesu alipowatuma mitume na kupitia kwao, kanisa, alisema, "na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" Mathayo 28:20. Kama tu vile Boazi aliwabariki wavunaji wake kwamba Yahweh atakuwa nao katika mavuno, vivyo tumebarikiwa na maneno ambayo Yesu alisema, Nipo nanyi siku zote. MIMI Nipo yupo nasi kila wakati katika mavuno! Ni mavuno ya mkate. Kuna mkate mwingi wa kuwa nao katika Nyumba ya Mkate!

Ndoa Bethlehemu

Boazi, Bwana wa mavuno, alikuja akawa jamaa wa kiume-mkombozi na mume mpya kwa Ruthu! Kuna ndoa mpya! Ni Bethlehemu ambapo ndoa hiyo ilifanyika! Watu walimwambia Boazi, "Yahweh na amfanye mwanamke huyu aingiaye nyumbani mwako kuwa kama Raheli na Lea, wale wawili walioijenga nyumba ya Israeli; nawe ufanikiwe katika Efrata na kuwa mashuhuri katika Bethlehemu… kwa wazao atakaokupa Yahweh katika mwanamke huyu" Ruthu 4:11-12. Boazi ni picha ya Kristo, Mkombozi, Bwana wa mavuno na Bwana harusi ambaye amewakaribisha Wayunani kuwa sehemu ya Mwili wake, Bi Harusi wake! Uzao wa ndoa hiyo alikuwa "Obedi, na Obedi akamzaa Yese; na Yese akamzaa Daudi" Ruthu 4:21-22. Ukoo wa Masiha inalelewa na kukua katika Bethlehemu!

DAUDI MFALME-Mfalme anakuja Bethlehemu

Baada ya Yahweh kumkataa Sauli kama mfalme wa Israeli, alimwambia nabii Samweli, "Ijaze pembe yako mafuta, uende, nami nitakupeleka kwa Yese, Mbethlehemu; maana nimejipatia mfalme katika wanawe"1 Samweli 16:1. Alitumwa kwa Yese, mtu kutoka Bethlehemu, Nyumba ya Mkate. "Samweli akafanya hayo aliyosema Yahweh, akaenda Bethlehemu"mst.4. Bethlehemu ni mahali pa Mfalme aliyepakwa mafuta wa Mungu! Mwishowe, Samweli akampata Daudi "na Yahweh akasema, Ondoka, umtie mafuta; maana huyu ndiye! Ndipo Samweli…akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya Yahweh akamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile"1Samweli 16:12-13. Upako wa kifalme unapatikana Bethlehemu. Upako wa Masiha unapatikana Bethlehemu. Nyumba ya Mkate ndiyo mahali pa upako wa kifalme! Mfalme anatoka Bethlehemu!

Mchungaji Mfalme anapatikana Bethlehemu

Daudi alikuwa mchungaji. "Basi Daudi alikuwa akienda kwa Sauli na kurudi ili awalishe kondoo za baba yake huko Bethlehemu"1Samweli 17:15. Kondoo hulishwa Bethlehemu! Mfalme ni mchungaji na anachunga kondoo za Baba yake! Yesu alisema, "Mimi ndiye mchungaji mwema" Yohana 10:11,14. Masiha, Mfalme aliyepakwa mafuta, ni mchungaji. Yeye na Baba ni mmoja (Yohana 10:30) na yeye huchunga kondoo zake na kutoa maisha yake kwa ajili yao! Yeye hulisha kondoo wake Bethlehemu, Nyumba ya mkate. Ni muhimu kwamba sisi, kama Petro

alivyotumwa na Yesu, pia tuonyeshe upendo wetu kwa Yesu kwa kulisha wanakondoo wake, kuchunga na kulisha kondoo wake (Yohana 21:15-17).

Bethlehemu huzaa wauaji wa Majitu!

Daudi alipokwenda nje kumwua jitu, Goliathi, Sauli alijibu kwa kumwambia kamanda wake, Abneri, "Je, Abneri, kijana huyu ni mwana wa nani?"1Samweli 17:56. Sauli alitaka kujua mahali kijana huyu alikuwa ametoka "Hata na Daudi alipokuwa yuarudi kutoka katika kumwua yule Mfilisti, Abneri alimtwaa, akamleta mbele ya Sauli naye anacho kichwa chake yule Mfilisti mkononi mwake. Basi Sauli akamwuliza, Wewe, kijana, u mwana wa nani? Naye Daudi akamjibu, Mimi ni mwana wa mtumishi wako, Yese, mtu wa Bethlehemu" mist.57-58. Daudi alitambua kwamba alitoka Bethlehemu! Tunapokua katika Nyumba ya Mkate tunakua kama "vijana, kwa sababu tuna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yetu, na tunamshinda yule mwovu"1 Yohana 2:14b. Vijana wana nguvu kwa sababu neno linakaa ndani yao! Ni katika Nyumba ya Mkate ndipo yunakuwa na nguvu kwa sababu tunashiriki katika Neno! Kama Daudi, basi tunaweza kumshinda yule mwovu! Tunakuwa na nguvu Bethlehemu tunapolishwa kwa Mkate wa uzima!

UNABII-Masiha kuzaliwa Bethlehemu!

Mika alitabiri, "Bali wewe, Bethlehemu, Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele"5:2. Mungu alichagua Bethlehemu Efrata; Nyumba ya Mkate na mahali pa kuzaa matunda, kuwa ndipo mahali ambapo atajidhihirisha katika mwili kama Mfalme! Masiha aliyezaliwa Bethlehemu ni "tangu milele" ambayo hasa kwa Kihibrania ni, "kutoka siku za milele". Mtawala anakuja kutoka Umilele. Yeye ndiye Wa milele, MIMI NDIYE, kuja katika mwili, kuzaliwa katika Nyumba ya Mkate!

Mfalme anapatikana na kuabudiwa Bethlehemu

Mamajuzi walikuja na kumpata Mtoto mchanga ambaye alikuwa Mfalme Bethlehemu kulingana na unabii (Mika 2:11). Walimpata Mfalme kati Nyumba ya Mkate. Watu leo wanafaa kumpata Masiha, Mfalme aliyepakwa mafuta, katika nyumba yake, ambayo ni nyumba ya mkate. Watu wanapoguzana na watu wa kanisa lake, wanatakikana kumpata "Kristo (Mfalme aliyepakwa mafuta) ndani yako; tumaini la utukufu" Wakolosai 1:27. Huu ndio Mkate wa Uzima, Upako wa Kifalme ambao unapatikana ndani ya nyumba yake. Katika Bethlehemu Yesu kama mtoto aliabudiwa! Yesu huabudiwa katika Nyumba ya Mkate! Neno la Mungu humfunua Kristo. Tunapokula na kulipokea neno lake tunamwona Yesu na tunaweza kumwabudu!

Mateso pia huja Bethlehemu

Mfalme Herode aliposikia habari za Masiha katika Bethlehemu "akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na waliopungua" Mathayo 2:16. Neno linapotokea nje eti Kristo anaanza kuonekana katika Nyumba ya Mkate kutakuwa na upinzani. Shetani hushambulia, hata kupitia serikali za wanadamu, kujaribu kusimamisha dhihirisho la Mungu katika mwili kufikia ukomavu. Hii inatimizwa katika unabii wa Yeremia kuhusu "Raheli akililia watoto wake" Mathayo 2:18. Yesu aliye Masiha ni Mwana wa huzuni na pia Mwana wa mkono wa kuume! Kuna mateso lakini pia kuna utukufu mwingi kupitia katika "kufufuliwa na kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu" Waefeso 2:6.

Tuko katika wakati ambao joka anataka kumrarua “mtoto wa kiume (hasa ‘mwana’) mara tu anapozaliwa” Ufunuo 12:4. Mtoto wa kiume “atatawala (hasa ‘kuchunga’) mataifa yote kwa fimbo la chuma. Na Mtoto wake akachukuliwa kwa Mungu na kwa kiti chake cha enzi” Ufunuo 12:5. Ni wakati wa Masiha wa pamoja kutokea! Mwana wa pamoja atajidhihirisha kuchunga mataifa yote, kufundisha mataifa yote! Huyu Masiha wa pamoja anatokea kutoka Bethlehemu, Nyumba ya Mkate. Kuna upinzani lakini hakuna kinachoweza kusimamisha kusudi la Mungu!

Tunafaa kuwa Nyumba ya Mkate!
Masiha anafaa kuonekana ndani yetu!
Upako wake wa Kifalme unafaa kupitiwa kati yetu!
Tumekombolewa, watenda kazi katika mavuno na kuunganishwa katika ndoa katika Nyumba ya Mkate!
Sisi, kanisa, ndio Bethlehemu wa kiroho!